



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI (NACTE)



TAARIFA KWA UMMA

MATOKEO YA UCHAGUZI WA PROGRAMU MBALIMBALI KWA MKUPUO  
WA SEPTEMBER KWA MWAKA WA MASOMO 2021/2022

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) ni chombo kilichoanzishwa kwa Sheria ya Bunge Sura ya 129, ili kusimamia na kuratibu utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo katika vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo. Jukumu mojawapo la Baraza ni kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa katika Vyuo vya Ufundi na Mafunzo nchini yanakidhi vigezo na ubora unaohitajika katika soko la ajira ndani na nje ya nchi. Katika kutekeleza jukumu hilo, Baraza linao wajibu wa kuratibu udahili wa wanafunzi kwenye Vyuo na kozi/programu zinazotambulika na mamlaka husika.

Udahili kwa mwaka wa masomo 2021/2022 ulianza tarehe **27 Mei, 2021** hadi tarehe **13 Agosti, 2021**. Waombaji wa kozi za Astashahada na Stashahada walituma maombi ya kudahiliwa katika Vyuo mbalimbali. Vyuo vilichagua waombaji wenye sifa kulingana na programu zinazotolewa. Waombaji **66,498** kutoka Vyuo **330** walichaguliwa kujiunga na programu mbalimbali na kisha kuwasilishwa NACTE kwa ajili ya uhakiki. Kati ya hao, waombaji **63,813** (96%) wamekidhi vigezo vya kujiunga na programu walizochagua na **2,685** (4%) hawakuwa na vigezo vya kujiunga kwenye programu walizochagua. Majina ya waombaji waliohakikiwa tayari yametumwa Vyuoni.

Waombaji wote waliowasilishwa NACTE kwa ajili ya uhakiki wametumiwa ujumbe na msimbo (*code*) kupitia simu na barua pepe zilizowasilishwa na Vyuo wakati wa kutuma maombi. Msimbo huo utatumika kuhakiki udahili wao na sifa kwenye kozi walizochaguliwa na Vyuo kupitia tovuti ya NACTE [www.nacte.go.tz](http://www.nacte.go.tz) kwa kubofya kitufe cha "**Verification results 2021**". Waombaji waliohakikiwa na sifa zao hazikukidhi vigezo vya programu wanashauriwa kuomba upya kwenye Vyuo na kozi kulingana na vigezo katika awamu ya pili itakayoanza **tarehe 17 hadi 29 Septemba, 2021**. Wito pia, unatolewa kwa wale ambao hawakuomba kufanya hivyo kwakuwa hakutakwepo na nafasi nyingine ya udahili kwa mwaka wa masomo 2021/2022. **Dirisha hili la awamu ya Pili halitahusu vyuo vya Afya vya Serikali.**

Aidha, majina ya waombaji wataochaguliwa katika awamu hii ya pili yatawasilishwa NACTE kwa ajili ya uhakiki kuanzia tarehe **23 Septemba, hadi 3 Oktoba, 2021**. Matokeo ya uhakiki yatatolewa ifikapo tarehe **15 Oktoba, 2021**. Masomo kwa waliochaguliwa yataanza rasmi tarehe **18 Oktoba, 2021**.

Hivyo, wanafunzi, wazazi na umma kwa ujumla wanashauriwa kuepuka kutapeliwa na wale wanaodai kwamba masomo yameanza kabla ya tarehe hiyo. Baraza pia linafuatilia kwa karibu kujua Vyuo vyote ambavyo vinakiuka taratibu na hatua kali zitachukuliwa dhidi yao. Kama kuna wanafunzi ambao tayari wameitwa kuanza masomo au wataitwa kabla ya tarehe 18 Oktoba, 2021 wawasiliane na Baraza kupitia barua pepe [admissions@nacte.go.tz](mailto:admissions@nacte.go.tz).

**IMETOLEWA NA:  
OFISI YA KATIBU MTENDAJI  
BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI (NACTE)  
TAREHE: 16/09/2021**